

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Mtaa wa Bagara Miyomboni,
S.L.P. 386,
27103 MANYARA,
Barua Pepe: rbcmanyara@pccb.go.tz.
www.pccb.go.tz

MANYARA – DESEMBA 24, 2020

TAARIFA KWA UMMA

**MALI ZILIZOKUWA ZINASHIKILIWA NA WAKOPESHAJI HARAMU
ZAREJESHA KWA WALIOATHIRIKA NA MIKOPO HIYO
MERERANI**

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro Mheshimiwa Eng. Zephania Adriano Chaula mnamo tarehe 24/12/2020 atakabidhi mali mbali mbali kwa waathirika wa mikopo umiza katika mji mdogo wa Mererani.

Mali hizo zinarejeshwa kutokana na jitihada za TAKUKURU Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara kuwasaidia wanyonge waliodhulumiwa mali zao kutokana na mikopo umiza ambapo mali zinazorejeshwa ni kama ifuatavyo;

Na.	MALI INAYOREJESHA	ANAYEREJESHEWA MALI	MKOPO ALIOCHUKUA (TZS)	DENI KWA SASA
1.	Nyumba tatu na Kadi ya pikipiki Na. T389BXE	Moses Mathayo Makala	1,500,000/=	43,000,000/=
2.	Mkataba mauziano ya nyumba	Bernady Lule Nyarasya	500,000/=	500,000/=
3.	Pikipiki na kadi yake Na. T848BNF	Godwin Mmasy	200,000/=	200,000/=
4.	Pikipiki Na. T966CRT	Jimmy Fedrick Kibindi	500,000/=	
5.	Gari OPEL VECTRA na kadi yake	Raphael Alex Ombade	5,200,000/=	
6.	Shamba la ekari tatu na nusu lililopo Migungani na mkataba wa kuweka shamba rehani	John Noel Laizer	2,500,000/=	4,700,000

7.	Gari Na. T161ATC* pamoja na kadi yake	Mohamed Abrahamu Matinda	500,000/=	500,000/=
8.			4,000,000/=	6,000,000/=
9.	Gari Toyota land Cruiser Na. T416AKK na Kadi yake.	Lengayen Sekeni Rumas	7,000,000/=	15,000,000/=
10.	Nyumba na nakala ya hati ya kiwanja	Yasinth Charles Adiro (Mrs. Ogola Owende)	10,300,000/=	10,300,000/=

Bada ya urejeshaji huu, ni vyema wananchi wakafahamu kuwa Sheria ya Biashara ya Fedha ya mwaka 2018 (The Microfinance Act, 2018) inatoa katazo kufanya biashara ya fedha kwa kutoza riba bila kuwa na leseni, Kifungu cha (16) cha Sheria hiyo kinatoa adhabu kali ya kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano kwa anayekiuka sheria hii.

Ni Rai yetu kwa watazania wote wenye nia ya kufanya biashara ya fedha, wafuate utaratibu wa kukata leseni ikiwa pamoja na kulipa kodi stahiki ili waweze kufanya biashara hii kwa mujibu wa sheria za nchi

Imetolewa na:

HOLLE J. MAKUNGU
MKUU WA TAKUKURU (M)
MANYARA